

REF: PPR/09- 1/11

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA TAREHE 12 SEPTEMBER 2011

Kulingana na Kanuni ya Kukokotoa bei za bidhaa za mafuta ya petroli bei zimekuwa zikikokotolewa na kutangazwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kila baada ya wiki mbili. EWURA inatangaza bei kikomo za mafuta ya petroli nchini zitakazoanza kutumika kuanzia **Jumatatu, Tarehe 12 Septemba 2011**. Bei hizi zimekokotolewa kwa kuzingatia kanuni mpya iliyoanza kutumika mwanzoni mwa Agosti 2011. Pamoja na kutambua bei elekezi/kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa aina zote za mafuta zimeshuka ikilinganishwa na bei zilizoanza kutumika kuanzia tarehe 29 Agosti 2011. Katika toleo hili bei za reja reja zimeshuka kama ifuatavyo: Petroli TZS 38.03 sawa na asilimia 1.84, Dizeli TZS 45.15 sawa na asilimia 2.26 na Mafuta ya taa TZS 46.15 sawa na asilimia 2.33. Mabadiliko haya ya bei za mafuta nchini yametokana na kushuka kwa bei ya mafuta katika soko la dunia kama ifuatavyo: Petroli asilimia 2.54, Dizeli asilimia 3.78 na Mafuta ya taa asilimia 3.50. Bei za mafuta katika soko la ndani zingeshuka zaidi isingekuwa kuendelea kushuka kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania ikilinganishwa na dola ya Marekani (sarafu ambayo hutumika katika manunuzi ya bidhaa za mafuta kwenye soko la dunia). Katika kipindi hicho, thamani ya shilingi ya Tanzania imeshuka kwa asilimia 0.20 ikilinganishwa na dola ya Marekani. Bei za jumla kwa kulinganisha matoleo haya mawili zimeshuka kama ifuatavyo: Petroli TZS 38.03 sawa na asilimia 1.90, Dizeli TZS 45.15 sawa na asilimia 2.34 na Mafuta ya Taa TZS 46.15 sawa na asilimia 2.41.
- (b) Bei za rejareja na za jumla zingepanda zaidi endapo formula ya zamani ingeendelea kutumika. Kwa kulinganisha vigezo vilivyo katika fomula ya zamani na fomula mpya, bei za mafuta zingekuwa kama ifuatavyo:

Aina ya Mafuta	Bei za Rejareja (TZS/L)		Bei za Jumla (TZS/L)	
	Kwa Formula ya zamani	Kwa Formula Mpya	Kwa Formula ya zamani	Kwa Formula Mpya
Petroli	2,205.27	2,031.54	2,137.01	1,964.04
Dizeli	2,126.35	1,954.17	2,053.78	1,886.67
Mafuta ya Taa	2,107.96	1,933.64	2,035.40	1,866.14

Kama inavyoonyesha kwenye jedwali hapo juu, formula mpya inaendelea kutoa unafuu kwa watumiaji ukilinganishwa na kama fomula ya zamani.

- (c) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2008, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (d) **Kampuni za mafuta zipo huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani ilimradi bei hizo ziko chini ya bei kikomo (price cap)** kama ilivyokokotolewa na *fomula* iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 5 la tarehe 9 Januari 2009 na marekebisho yaliyofanywa kupitia Tangazo ya Serikali Na. 216 la Tarehe 29 Julai 2011.
- (e) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionyesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta kutoka kwenye vituo vinavyouza mafuta kwa bei ndogo zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja na adhabu itatolewa kwa kituo husika.**
- (f) Wanunuzi wanashauriwa kuhakikisha kuwa wanapata stakabadhi ya malipo inayoonesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hiyo ya malipo itatumika kama kidhibiti cha mnunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya ama kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo; ama endapo utakuwa umeuziwa mafuta yenye kiwango cha ubora kisichofaa.

A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Elekezi		
	Petroli (TZS/LT)	Mafuta ya Taa (TZS/LT)	Dizeli (TZS/LT)
Dar es Salaam	2,032	1,934	1954
Arusha	2,116	2,018	2038
Arumeru	2,116	2,018	2038
Karatu	2,134	2,036	2056
Monduli	2,121	2,023	2043
Ngorongoro (Loliondo)	2,193	2,095	2115
Kibaha	2,036	1,938	1959
Bagamoyo	2,043	1,945	1965
Kisarawe	2,039	1,941	1961
Mkuranga	2,041	1,943	1964
Rufiji	2,059	1,961	1982
Dodoma	2,090	1,992	2013
Konooa	2,123	2,025	2045
Kongwa	2,088	1,990	2010
Mpwapwa	2,092	1,994	2014
Iringa	2,096	1,998	2018

Kilolo	2,100	2,002	2023
Ludewa	2,162	2,064	2084
Makete	2,155	2,057	2077
Mufindi	2,105	2,007	2028
Njombe	2,124	2,026	2046
Bukoba	2,247	2,149	2169
Biharamulo	2,221	2,123	2143
Karagwe	2,263	2,165	2185
Muleba	2,238	2,140	2160
Ngara	2,179	2,081	2101
Misenyi	2,255	2,157	2177
Kigoma	2,263	2,165	2185
Kasulu	2,249	2,151	2171
Kibondo	2,227	2,129	2149
Moshi	2,105	2,007	2028
Hai	2,108	2,010	2031
Mwanga	2,098	2,000	2021
Rombo	2,127	2,029	2049
Same	2,091	1,994	2014
Siha	2,112	2,014	2034
Lindi	2,090	1,992	2013
Kilwa Masoko	2,065	1,967	1988
Liwale	2,112	2,014	2034
Nachingwea	2,120	2,022	2042
Ruangwa	2,118	2,020	2040
Babati	2,154	2,056	2076
Hanang	2,165	2,067	2087
Kiteto	2,165	2,067	2087
Mbulu	2,167	2,069	2089
Simanjiro	2,186	2,088	2108
Musoma	2,210	2,112	2132
Bunda	2,201	2,103	2123
Serengeti	2,256	2,158	2178
Tarime	2,221	2,123	2143
Mbeya	2,138	2,040	2061
Chunya	2,148	2,050	2071
Ileje	2,152	2,054	2074
Kyela	2,154	2,056	2077
Mbarali	2,123	2,025	2045
Mbozi	2,148	2,050	2070
Rungwe	2,147	2,049	2070
Morogoro	2,057	1,959	1979
Mikumi	2,072	1,974	1995

Kilombero	2,095	1,997	2017
Mahenge	2,105	2,007	2027
Kilosa	2,075	1,977	1997
Mvomero	2,067	1,969	1989
Mtwara	2,104	2,006	2026
Masaki	2,129	2,032	2052
Newala	2,136	2,038	2058
Tandahimba	2,129	2,031	2051
Mwanza	2,181	2,083	2104
Geita	2,223	2,125	2145
Kwimba	2,218	2,120	2140
Magu	2,189	2,091	2112
Misungwi	2,187	2,089	2110
Sengerema	2,214	2,116	2136
Ukerewe	2,241	2,143	2163
Sumbawanga	2,205	2,107	2127
Mpanda	2,239	2,141	2161
Nkasi	2,218	2,120	2140
Songea	2,155	2,057	2077
Mbinga	2,189	2,091	2111
Namtumbo	2,184	2,086	2106
Tunduru	2,214	2,116	2136
Shinyanga	2,160	2,062	2083
Kahama	2,174	2,076	2096
Bukombe	2,186	2,088	2109
Bariadi	2,202	2,104	2124
Kishapu	2,189	2,091	2111
Maswa	2,193	2,095	2115
Meatu	2,200	2,102	2122
Singida	2,122	2,024	2045
Iramba	2,134	2,036	2057
Manyoni	2,107	2,009	2029
Tabora	2,186	2,088	2108
Igunga	2,139	2,042	2062
Nzega	2,150	2,052	2073
Sikonge	2,198	2,100	2120
Urambo	2,199	2,101	2121
Tanga	2,078	1,980	2000
Handeni	2,069	1,971	1991
Kilindi	2,092	1,994	2014
Korogwe	2,071	1,973	1993
Lushoto	2,081	1,983	2003
Mkinga	2,092	1,994	2014

Muheza	2,078	1,980	2000
Pangani	2,084	1,986	2007

B: BEI ZA JUMLA

Bei za Jumla - DSM	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Bei Kikomo	1,964.04	1,886.67	1,866.14

Haruna Masebu
MKURUGENZI MTENDAJI
EWURA